SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI na MATUKIO Gazeti

Julai 07, 2021



Gazeti la Reli | Toleo Namba 15 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## RAIS SAMIA AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhandisi Robert Gabriel Luhumbi, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Dkt. Leonard Chamuriho, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa pamoja na viongozi wengine wa Chama, Serikali na Bunge, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa kipande cha Mwanza - Isaka.**

Na Mwandishi wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR ) kipande cha Mwanza – Isaka Fela jijini Mwanza Juni, 2021.

Akihutubia wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya Mwanza - Isaka yenye urefu wa kilometa 341 ambao utagharimu kiasi cha Shilingi Trilioni 3.06, amesema mradi huo utaongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kusafirisha kwa haraka na kwa kiwango kikubwa cha mizigo na watu tofauti na ilivyo sasa.

Mhe. Rais Samia ameeleza kuwa mradi huu ni sehemu ya mradi mkubwa wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilomita 1,605 ambao utatengeneza ajira 11,000 hivyo kuwataka wakazi wa Mwanza kuchangamkia fursa ya ujenzi wa reli hiyo kwa kuwa wavuvi, wakulima na wafugaji watanufaika na reli hiyo ambayo itakuwa na behewa maalumu ya kubebea mazao, nyama na samaki.

“Nitoe wito kwa wakazi wa Mwanza miradi hii inayotekelezwa imekuja na fursa za ajira na biashara hivyo hakikisheni mnatumia fursa hii vizuri, hapo mbele tunaambiwa kuna kambi inajengwa lakini kuna

Inaendelea Uk. 2

# RAIS SAMIA AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA

Na Mwandishi wetu

Inatoka Uk. 1



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la mradi huo katika sherehe zilizofanyika Fela mkoani Mwanza Juni, 2021.

makambi kadhaa yameshajengwa ndani ya mkoa huu, makambi yote hayo yanataka kula na kunywa na huduma nyingine ambazo ninyi wanamwanza na wengine mnatakiwa kutumia fursa hizo kuimarisha uchumi na biashara zenu"

Aidha, amesema reli hiyo itapunguza muda wa kusafiri kati ya Mwanza hadi Dar es Salaam kutoka saa 17 za sasa kwa usafiri wa mabasi hadi saa 8 mradi utakapokamilika.

Mhe. Samia ameongeza kuwa tayari Serikali imeanza kujipanga kwa ajili ya kumalizia vipande vya Makutupora – Tabora na Tabora – Isaka ili kukamilisha awamu ya kwanza na baadaye kuendeleza mradi huo katika maendeo mengine ya nchi na nchi jirani za Rwanda, Congo, Uganda na Burundi.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa ameeleza kuwa utekelezaji wa mradi wa SGR kipande cha Mwanza – Isaka ni sehemu ya ukamilishaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza ambao una vipande vitano vikiwemo Dar es Salaam – Morogoro ambacho kimefikia 92% na Morogoro – Makutupora ambacho kimefikia 62%.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Leonard Chamuriho wakifurahia mara baada ya kuweka jiwe la msingi la Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha tano (5) Mwanza – Isaka katika hafla ya uzinduzi Fela jijini Mwanza Juni 2021.

# MARAIS WASTAAFU WAPONGEZA UTEKELEZAJI WA MRADI WA RELI YA KISASA

Na Mwandishi wetu



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) akiwaelezea Marais Wastaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Morogoro - Makutupora walipotembelea mradi huo Kilosa mkoani Morogoro, Julai 2021.

Marais Watsaafu pamoja na Mawaziri Wakuu Wastaafu wafanya ziara ya siku moja kukagua Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kuanzia Kilosa mkoani Morogoro hadi jijini Dar es Salaam, Julai 06, 2021.

Marais Wastaafu walioshiriki ziara hiyo ni Rais wa awamu ya pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi na Rais Mstaafu wa awamu ya Nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete wakiambatana na Mawaziri Wakuu Wastaafu Mhe. John Malecela na Mhe. Mizengo Peter Pinda pamoja na viongozi mbalimbali wakiwemo wakuu wa mikoa na Wilaya ambazo mradi wa SGR unapita katika maeneo yao.

Lengo la ziara hiyo ni kuona kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ambayo utekelezaji wake ni mipango iliyowekwa na Marais wa awamu zilizopita.

Marais hao waliweza kuona maendeleo ya mradi ambapo walitembelea Handaki lenye urefu wa zaidi ya Kilometa moja lililopo Kilosa mkoani Morogoro, Stesheni za SGR za Morogoro, Ngerengere, Soga na kuhitimisha ziara yao katika jengo la Tanzanite ambalo ni Stesheni kuu ya SGR jijini Dar es Salaam.

Waheshimiwa Marais Wastaafu wakiwa ndani ya treni ya Uhandisi inayomilikiwa na mkandarasi Yapi Merkezi walipata fursa ya kujionea kazi mbalimbali zikiendelea ambazo kwa kiasi kikubwa ni kazi za kuhitimisha Mradi huo kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho kimefikia zaidi ya 92%.

Marais Wastaafu walionesha kuridhishwa na kufurahishwa na jitihada za serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Samia kupitia Shirika la Reli Tanzani – TRC kwa utekelezaji na usimamizi wa mradi huo huku wakieleza faida ambazo nchi itazipata kupitia mradi huo katika nyanja ya Kijamii na kiuchumi.=

“Tunamshukuru muasisi wa kazi hii Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kwa fikra njema, kwani kila jambo linaanza na fikra, kafanya kazi nzuri pamoja na awamu ya sita ambayo Mhe. Samia Suluhu Hassan ameanza vizuri kwa kuendeleza yale ambayo walikuwa wanayafanya na mwenzie, pia namuombea aweze kuendelea kufanya yale mazuri waliyoanzisha” amesema Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa awamu ya pili

Rais Mstaafu wa awamu ya nne Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete amesema kuwa amefurahishwa kuona mipango iliyopangwa na Marais waliotangulia inatekelezwa kwani mpango wa kujenga reli ulikuwepo tangu kipindi cha Hayati Benjamin William Mkapa, Rais wa awamu ya tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliweka mpango wa kujenga reli kwa kiwango cha kimataifa kutoka Dar es Salaam - Isaka hadi Kigali, Isaka – Mwanza, Tabora - Kigoma na Kaliua – Kalema.

“Jambo la faraja ni kwamba tunapata reli ya kisasa yenye uwezo wa kubeba mzigo mkubwa zaidi na abiria wengi, hili ni jambo la kufurahisha na kuwashukuru wote waliotoa wazo la kuwa na reli ya namna hii lakini kubwa zaidi ni kwa wale waliothubutu”

Mhe. Rais Mstaafu Kikwete aliongeza kuwa Mradi huu utasaidia kupunguza muda wa safari na kuongeza ufanisi katika ubebaji mizigo na abiria na kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi kwa kurahisisha shughuli za kijamii na kiuchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa amewashukuru Marais Wastaafu na Mawaziri Wastaafu kwa kutembelea Mradi wa SGR kwa kuwa usanifu wa mradi huo ulianza kipindi cha Hayati Benjamini Mkapa hivyo watanzania watarajie mambo mazuri kwa mradi huo unaendelea vizuri na hivi karibuni huduma zinatarajiwa kuanza kutoa huduma.

# TRC YASHIRIKI KONGAMANO LA SIKU 100 ZA MHE. RAIS SAMIA

Na Mwandishi wetu




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (wa pili kulia katika meza kuua) akieleza mafanikio ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya reli wakati wa Kongamano la siku 100 za Mhe. Rais Samia katika ukumbi wa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwl. Nyerere Juni,

Shirika la Reli Tanzania – TRC laadhimisha siku 100 za Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushiriki Kongamano la siku 100 za Mhe. Samia lililoandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara - TNBC katika ukumbi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mwl. Nyerere Juni, 2021.

Kongamano hilo limefanyika kwa lengo la kuwakutanisha wadau mbalimbali wa maendeleo kutoka Sekta binafsi, taasisi na mashirika ya umma kueleza na kujadili mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha siku 100 za Mhe. Samia Suluhu pamoja na kuona namna bora ya kuendeleza mazuri yaliyofanyika ndani za siku 100 za Mhe. Samia.

Mgeni Rasmi katika kongamano hilo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akifungua kongamano hilo amesema "Nawashukuru sekta binafsi kwa kuendelea kuunga mkono serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe Rais Samia, naomba ushirikiano huu uendelee ili kwa pamoja tuweze kusonga mbele kwa kasi na kuendelea mbele" alieleza Mhe. Kassim

Akieleza baadhi ya mafanikio ya Mhe. Rais Samia Suluhu, Waziri Mkuu amesema kuwa Mhe. Rais ameendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo inaendelea kujengwa ikiwemo Reli ya Kisasa – SGR kutoka Dar es Salaam kuelekea Morogoro hadi Makutupora Singida pamoja na kipande cha kutoka Isaka hadi Mwanza.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa alieleza majukumu ya Shirika ambayo ni usafirishaji wa mizigo na abiria pamoja na uendelezaji wa miundombinu ya reli kwa kukarabati na kujenga ambapo hivi sasa Shirika limejikita zaidi katika kujenga miundombinu mipya,

Kadogosa alisema kuwa "Katika kipindi cha siku 100 mradi wa SGR unaendelea vizuri ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro kimefika 92% na Morogoro – Makutupora Singida kimefika zaidi ya 62%, Mhe. Rais ameidhinisha Shilingi Bilioni 376.34 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli Mwanza – Isaka ambapo jiwe la msingi liliwekwa Juni 14, 2021 na ujenzi wake umeshaanza, pia Mhe. Rais ameelekeza kuanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Makutupora hadi Isaka".

# VIONGOZI MBALIMBALI WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI WASIFU MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu

Viongozi mbalimbali kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki waisifu nchi ya Tanzania pamoja na Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa utekelezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR walipotembelea mradi kuanzia stesheni ya Dar es Salaam hadi Pugu, Juni 25, 2021.

Viongozi hao ni pamoja na wakurugenzi mbalimbali, wawakilishi wa makatibu wakuu wa Jumuiya ya Afika Mashariki kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani Kusini na Balozi wa Sudani Kusini Tanzania ambapo wamepata fursa ya kuona maendeleo ya mradi wa SGR na ufanisi mkubwa uliotumika katika ujenzi huo.

Pia viongozi hao walitembelea katika kituo cha kwanza chenye mitambo ya kupoozea umeme kilichopo katika eneo la Pugu na kupata maelezo juu ya mitambo hiyo itakavyoweza kufanya kazi kudhibiti umeme mkubwa na kupeleka kiwango cha umeme utakaohitajika kwenye uendeshaji wa treni.

Mkurugenzi wa huduma ya Usambazaji Hewa kutoka katika Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini Sudani Kusini Bw. Stephen Rombe amefurahishwa sana kuona maendeleo ya ujenzi wa mradi huo mkubwa na kusema kuwa mradi huo utafika mbali hadi kufikia katika mipaka ya nchi jirani kwa ajili ya kukuza uchumi katika nchi za Afrika Mashariki na kati.

"Tanzania imefanya kitu kikubwa ambacho jumuiya za nchi nyingine za Afika zinatakiwa kufanya miradi mikubwa kama huu" alisema Bw. Rombe.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Miundombinu ya Ujenzi TRC Mhandisi Faustine Kataraia amesema kuwa ziara hiyo ni muhimu sana kwa TRC kwa kupata ugeni kutoka nchi za Afrika kwa kutambua kitu kinachofanywa na TRC katika kuimarisha miundombinu ya reli.

Mhandisi Kataraia ameeleza kuwa miundombinu ya reli itaimarisha uchumi wa nchi ya Tanzania pamoja na nchi jirani kwa usafirishaji wa mizigo na pia itasaidia kulinda barabara kwa kupitisha mizigo yenye uzito mkubwa kwa njia ya treni




Mkurugenzi wa Miundombinu ya Ujenzi TRC Mhandisi Faustin Kataraia akiwaelezea baadhi ya wajumbe kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Stesheni ya SGR iliyopo jijini Dar es Salaam Juni, 2021.

# KAMPENI YA UELEWA KWA JAMII KUHUSU MRADI WA UJENZI WA SGR, MWANZA – ISAKA YAPIGA HODI KWIMBA MKOANI MWANZA



Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania – TRC linaendelea na kampeni maalum ya kutoa elimu ya uelewa kuhusu Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa SGR, kipande cha tano, Mwanza – Isaka (Km 341), kwa jamii zinazoishi maeneo ya kanda ya ziwa.

Kufuatia kampeni hiyo timu ya mawasiliano kutoka Shirika la Reli Tanzania TRC, imetembelea ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza ikiwa ni sehemu ya hatua muhimu ya Utekelezaji wa mradi kwa kuhakikisha uelewa Sahihi kwa viongozi na Wananchi juu ya masuala yanayohusu mradi ili kuifikia shabaha ya maendeleo ya Mtanzania mmoja mmoja na taifa kwa ujumla kupitia uimarishwaji wa sekta ya miundombinu ya Reli nchini.

Aidha wataalam hao kutoka vitengo mbalimbali vya Shirika la Reli Tanzania, walipata nafasi ya kuwasilisha ujumbe wa Kampeni hii katika kikao cha maandalizi ya Mapokezi ya mbio za Mwenge Wilayani Kwimba, kilichoongozwa na Mkuu wa wilaya ya Kwimba Mhe.Johari Samizi na kuhudhuriwa na Kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya, viongozi wa ngazi ya Wilaya na Kata pamoja na Taasisi binafsi.

Akiwatambulisha wataalamu hao katika kikao hicho, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk, ameeeleza kuwa lengo hasa la kufika katika kikao hicho, ni kufikisha ujumbe wa kampeni ya Uelewa Kuhusu mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa, na Kuhakikisha viongozi wanakuwa na Uelewa sahihi wa masuala yanayohusu mradi ili kurahisisha elimu kuwafikia Wananchi na hatimaye kurahisisha hatua zinazofuata katika Utekelezaji wa mradi, ikiwemo zoezi la utwaaji ardhi.

Kwa upande wake meneja Mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa SGR kipande cha Mwanza hadi Isaka, Mhandisi Machibya Masanja ameeleza kuwa utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati unaenda sambamba na faida mbalimbali ikiwemo fursa za ajira za moja kwa moja 11,000, akiongeza kuwa Zaidi ya watu 75,000 watanufaika na ajira zisizo za moja kwa moja.

Kwa upande mwingine, viongozi hao waliweza kupata nafasi ya kuuliza maswali juu ya masuala mbalimbali yanayohusu mradi ikiwemo fidia na Utwaaji ardhi, ambapo Afisa Mwandamizi kutoka Kitengo cha Ardhi TRC Bw. Fredrick Kusekwa ameeleza kuhusu taratibu na Sheria zinazoongoza zoezi la utwaaji ardhi sambamba na sifa za anayestahili kulipwa fidia.



Mkuu wa wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi, akieleza namna watakavyoshirikiana na TRC kufikisha ujumbe wa Kampeni ya Uelewa kwa Jamii kuhusu Mradi wa SGR wakati wa kikao cha viongozi wa wilaya ya Nyamagana katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza Julai, 2021.



Mkuu wa wilaya ya Nyamagana Mhe. Amina Makilagi, akizungumza jambo na meneja Mradi wa SGR, Mwanza - Isaka, Mhandisi. Machibya Masanja, baada ya Kikao cha Viongozi wa wilaya ya Nyamagana, katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza Julai, 2021



Meneja Mradi wa SGR Mwanza - Isaka, Mhandisi Machibya Masanja, akimfafanulia Mkuu wa Wilaya ya Misungwi Mhe. Veronica Kessy (watatu kutoka kushoto, Meza kuu) kuhusu Teknolojia inayotumika katika ujenzi wa Reli ya kisasa, wakati wa kikao cha Viongozi wa Wilaya hiyo Mkoani Mwanza Juni, 2021

# KAMPENI YA UELEWA KWA JAMII KUHUSU MRADI WA UJENZI WA SGR, MWANZA – ISAKA YAPIGA HODI KWIMBA MKOANI MWANZA

Na Mwandishi wetu



Baadhi ya wataalamu wanaounda timu ya mawasiliano kutoka TRC (kutoka kushoto, waliokaa) Mtaalamu wa masuala ya Mazingira Bi. Magdalena Kitila, Afisa Mwandamizi kutoka Kitengo cha Ardhi Bw. Fredrick Kusekwa na Meneja Mradi SGR, Mwanza - Isaka Mhandisi. Machibya Masanja, wakiwa katika mahojiano juu ya kampeni ya uelewa wa jamii kuhusu Mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa SGR Mwanza - Isaka, kupitia Kipindi cha Morning Express cha Kituo cha Redio cha City Fm jijini Mwanza, hivi karibuni Julai 2021.

Aidha Bw. Kusekwa ameeleza kuwa, katika utekelezaji wa mradi huu wenye thamani ya zaidi ya Sh. Trilioni 3. za Kitanzania, kila ambaye eneo lake litatwaliwa kwaajili ya ujenzi, atalipwa kulingana na anavyostahili.

Akizungumza baada ya ujumbe huo kutoka Shirika la Reli Tanzania, Mkuu wa Wilaya ya Kwimba Mhe. Johari Samizi, amewashukuru wataalam hao kutoka TRC na kuahidi ushirikiano wa dhati kwa kipindi chote ambacho mikutano ya hadhara ya Kampeni hiyo itakuwa ikifanyika Wilayani Kwimba.

"Tunafahamu watakwenda kukutana na viongozi wa ngazi za chini na wananchi wa hapa Kwimba ambao ndio wamiliki wa hayo maeneo, lakini sisi kwa ngazi ya Wilaya tutahakikisha kunakuwa na ulinzi na usalama kwa timu hii, ili kazi ifanyike kama ilivyokusudiwa"

Mbali na Mikutano ya hadhara na Wanachi, ili kufikisha ujumbe kwa ufanisi Zaidi, kampeni hii ambayo ni endelevu vilevile inafanyika kupitia vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii, amabapo kwa hatua hii ya awali, mikutano ya hadhara inafanyika katika mikoa ya Mwanza, Simiyu na Shinyanga.



Mkuu wa wilaya ya Kwimba Mhe. Johari Samizi, akitoa neno la shukrani kwa timu ya Mawasiliano ya Shirika la Reli Tanzania (waliokaa, kulia) baada ya timu hiyo kutoa elimu juu ya masuala yanayoambatana mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa SGR Mwanza - Isaka, katika kikao kilichohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa ngazi ya Wilaya hadi Kata, hivi Karibuni Julai, 2021



Daraja lenye urefu wa Mita 487.4 likiwa katika hatua za mwisho za ujenzi wake ambapo Daraja hili litaunganisha Handaki namba 2 na upande wa pili wa mto Mkondoa.



Muonekano wa sehemu ya maegesho ya Magari na Mabasi ya abiria yakiwemo ya Mwendokasi (BRT) nje wa Jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam ambayo ujenzi wake ukiwa katika hatua za mwisho.



Meneja Msaidizi wa Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Christopher John akiwapatia maelezo maafisa wa jeshi kuhusu ujenzi wa kituo cha SGR kilichopo Kilosa mkoani Morogoro hivi karibuni Juni, 2021.



Mkuu wa Kambi ya Jeshi Mikumi Kanali Christian Paul Mahundi (aliyevalia koti la kijivu), Meneja Msaidizi Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora (wa sita kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na maafisa wa jeshi mbele ya Handaki namba mbili Kilosa mkoani Morogoro, hivi karibuni Juni 2021.



Mhandisi wa Umeme Shirika la Reli Tanzania - TRC Yusuph Katuga akiwaelezea wananchi waliotembelea banda la TRC kuhusu mifumo ya umeme katika mradi wa SGR katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea katika viwanja vya Mw. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam Juni 2021.



Meneja wa Huduma kwa Wateja Shirika la Reli Tanzania - TRC Bi. Catherine Mushi (kulia) akimuelezea Bi. Anna Mose kuhusu huduma za treni katika mradi wa SGR alipotembelea banda la TRC katika Maonesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea katika viwanja vya Mw. Nyerere barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam Juni 2021.

Na Mpiga Picha wetu





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akisoma orodha ya majina ya viongozi mbalimbali walioshiriki kufanikisha kuanza kwa mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kipande cha Mwanza - Isaka kabla ya kuweka jiwe la msingi la mradi huo katika sherehe zilizofanyika Fela mkoani Mwanza tarehe 14 Juni, 2021.

## UJENZI WA KAMBI ZA MRADI WA RELI YA KISASA - SGR MWANZA - ISAKA









Kazi ya ujenzi wa Kambi ya Mradi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka ikiendelea Fela mkoani Mwanza, Mradi wa SGR Mwanza - Isaka utakuwa na Kambi kubwa nne ambazo ni Fela, Bukwimba, Malampaka na Lohumbo.

# TRC YASHIRIKI MAONESHO YA 45 YA KIMATAIFA YA BIASHARA - SABA SABA



Na Mwandishi wetu TRC




Hassan Mbonde, Afisa Uhusiano Shirika la Reli Tanzania - TRC akimueleza Bwana Jonas John kuhusu maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR alipotembelea banda la TRC katika viwanja vya maonesho Saba Saba jijini Dar es Salaam Juni 2021.

Shirika la reli Tanzania – TRC lashiriki maonesho ya kimataifa ya 45 ya biashara katika viwanja vya saba saba vilivyopo Kurasini Dar es Salaam kuanzia tarehe 01 - 13 Julai 2021.

Malengo ya maonesho hayo ni kutangaza huduma na bidhaa za kampuni na taasisi binafsi na za serikali, kuwakutanisha watoa huduma na wateja pamoja na kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma na bidhaa.

Kupitia maonesho haya Shirika linatoa elimu kuhusu miradi mikubwa inayosimamiwa na TRC ambayo ni ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Dar es salaam – Morogoro ambao umefika zaidi ya 92% na kipande cha Morogoro – Makutupora ambao umefika zaidi ya 62%, Mwanza - Isaka ambao ujenzi wake umeanza hivi karibuni na mradi wa uboreshaji wa reli ya kati – TIRP ambao umekamilika kwa 100%, kutoa huduma ya ukataji tiketi za treni pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa wadau.

Baadhi ya wageni waliotembela banda la TRC ni wanafunzi kutoka shule ya kimataifa ya Moshi, ambapo Wanafunzi hao wamevutiwa na namna Shirika linavyofanya shughuli zake hususani katika usimamizi wa miradi ya ujenzi.

Mmoja wa wanafunzi hao Asha Juma amesema kuwa "Mimi nataka kuwa Mhandisi natamani sana kujua jinsi gani ujenzi huu unafanyika, madaraja , reli na vitu vingine katika reli hii, na hamu yangu ni kuja kupanda treni hii itakapomalizika" Alisema mwanafunzi.

Shirika linawakaribisha wananchi wote kutembelea banda la TRC ili waweze kupata fursa ya kujifunza na kufahamu fursa zilizopo katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa.

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA KATIKA SIKU 100 ZA MHE. RAIS SAMIA SULUHU HASAN

Na Mwandishi wetu TRC




Shirika la Reli Tanzania limeeendelea kupata mafanikio mengi makubwa hususani katika kipindi cha siku 100 za uongozi wa Rais awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa serikali kuendelea kuona umuhimu wa miundombinu ya reli katika kukuza sekta ya usafirishaji kwa njia ya reli ambayo itawezesha usafiri wa reli kuwa wa uhakika na kuaminika zaidi.

Ndani ya siku 100 za Mhe. Rasi Sami Suluhu Hassan Serikali imeliwezesha Shirika kumalizia ukarabati Vichwa 7 sogeza na kuanza kutumika ambavyo vimeongeza ufanisi katika kupanga treni na kupunguza mzigo katika bandari ya Dar es Salaam na kuleta urahisi wa mizigo kufika kwa haraka katika sehemu husika , hivyo wananchi kuwa na imani ya kusafirisha mizigo yao kwa wingi na sekta ya usafirishaji kwa njia ya reli kuzidi kuingiza kipato cha nchi.

Shirika la Reli Tanzania limeendelea kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambacho ujenzi wake umefika zaidi ya asilimia 92% pamoja na kipande cha Morogoro – Makutupora ambacho ujenzi wake umefika zaidi ya asilimia 62%.

Aidha, Shirika limeendelea na hatua za awali za maandalizi ya ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Mwanza hadi Isaka chenye urefu wa KM 341 ambapo katika kipindi cha siku mia moja za Rais Samia, Serikali imeweza kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 372.34 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo ambao ujenzi wake umekwishaanza baada ya jiwe la msingi la mradi kwa kipande hiko kuwekwa.

Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR Mwanza – Isaka ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi mkubwa wa kimkakati wa SGR ambao unatekelezwa kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye jumla ya vipande vitano, Kipande cha kwanza Dar es salaam - Morogoro Kilomita 300, kipande cha pili Morogoro - Makutupora Kilomita 422, kipande cha tatu Makutupora - Tabora Kilomita 371, kipande cha nne Tabora - Isaka Kilomita 162 na kipande cha tano ni Isaka - Mwanza Kilomita 341.

Mkataba wa Ujenzi wa Mradi wa SGR Mwanza - Isaka umesainiwa kati ya Shirika la Reli Tanzania - TRC na ubia wa kampuni mbili za Kichina 'China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) na China Railway Construction Corporation Limited (CRCC)' mapema mwezi Januari 2021.

Kwa upande mwingine serikali imeendelea kusimamia ukarabati wa Behewa za mizigo ili kuhakikisha huduma ya usafirishaji mizigo unaimarika ambapo mpaka sasa jumla ya Behewa 193 kati ya 200 tayari zimekarabatiwa ambapo zitaleta tija katika ufanisi wa kazi kwa kuongezeka kwa awamu nyingi za safari za treni ya abiria na mizigo katika reli yetu ya kati.

Hata hivyo, TRC inaendelea na taratibu za uandaaji wa nyaraka kwa ajili ya ununuzi wa mkandarasi ili kutekeleza ujenzi wa reli ya Tabora – Kaliua - Mpanda hadi karema, reli hii ina urefu wa KM 317 na itaunganisha bandari ya Dar es Salaam na Karema, sambamba na hayo ndani ya siku 100 Serikali ya awamu ya sita imeahidi kuendelea kufadhili miradi ya uendelezaji wa reli nchini.

Shirika linajivunia na linatarajia mengi mazuri yatakayokuza miundombinu ya reli katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita kinachoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hasan kwa kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa reli ya kisasa ambao unaendelea pamoja na kuzidi kukuza usafiri wa treni kwa lengo la kupunguza adha ya usafiri nchini Tanzania.




**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**

**Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano**
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko** |
| **KIBONZO** | **Hassan Said** |
| **MTAYARISHAJI** | **Sami Omary** |

**tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz**
**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**